

# JINSI YA KUFUNGUA MIRATHI

## SHUGHULI ZA MIRATHI MAHAKAMANI

### MAHAKAMA YA MWANZO

Mirathi ya thamani ya shs. Millioni 5 isi-yoondosheka + million 3 inayoondosheka.

### MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI/WILAYA

Mirathi ya thamani ya shs. million 12 isiyoondosheka na milioni 10 inayoondosheka.


### MAHAKAMA KUU

Mirathi inayozidi milioni 12 + milioni 10. Mahakama Kuu hama kikomo.

## Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA  
(DESIGN AND DRAWING)  
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA  
NA ROYAL DANISH EMBASSY  
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT  
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA  
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

## A. WOSIA UKIWEPO

1. Mtu akifa, kifo kiandikishwe kwa Mkuu wa wilaya katika muda wa siku 30.
2. Anayetegemea kusimamia mirathi akafungue mirathi mahakamani akiwa na:
  - wosia uliachwa na marehemu
  - cheti cha kifo

(Msimamizi anaweza kufungua mirathi katika mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya wilaya Mahakama ya Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu kufuatana na thamani ya mali).

3. Mahakama kutoa tangazo la Mirathi kwa muda wa siku 90. Kama hakuna pingamizi lolote msimamizi hukabidhiwa barua ya kumhalalisha kugawa urithi na kilupa madeni.
4. Msimamizi hugawa mali kwa kufuata wosia unavyoelekeza.
5. Baada ya ugawaji msimamizi hurejesha nakala ya ugawaji mahakamani ili jalada lifungwe.

## KUMBUKA

Wengi hawarejeshi nakala ya ugawaji wa mali mahakamani. Hayo ni makosa kisheria na unaweza kushtakiwa. Barua ya kuomba usimamizi wa mirathi (sisitiza) lazima itaje.

- Juhudi zilizofanywa kuhakikisha kwamba marehemu hakuacha wosia.
- Maelezo kuhusu maskani yake.

## MUHIMU KUFANYWA NA KUZINGATIA (MSI-MAMIZI)

- Gharama za mazishi ziwe za kuridhisha kufuatana na hali ya marehemu.
- Gharama za usimamizi.
- Gharama za huduma alizozipata marehemu za aina yoyote.
- Madeni mengineyo.

## WAJIBU WA MSIMAMIZI WA MIRATHI

- Kukusanya madeni na mali za marehemu.
- Kulipa madeni ya marehemu.
- Kugawa mali yamarehemu kwa misingi ya haki.
- Kutayarisha "Inventory" (taarifa ya awali) na kuiwakilisha mahakamani. "Inventory (taarifa ya awali) itakuwa na vipengele vifuatavyo.
  - (i) maelezo ya mirathi ikielezea waziwazi mali na thamani ya mali za marehemu.
  - (ii) madeni.
  - (iii) matumizi.
  - (iv) jinsi mali iliyobaki na jinsi ilivyogawiwa kwa warithi.

- Hali na aina za mali za marehemu.
- Majina na anuani za wasimamizi.
- Maskani ya marehemu (muhimu!)
- Mirathi hufunguliwa kufuatana na maskani ya marehemu).
- Viambatanisho: Cheti cha kifo, Wosia.

## B. BILA WOSIA

1. Kifo kiandikishwe kwa Mkuu wa wilaya katika muda usiozidi siku 30.
  2. Mkutano wa Ukoo ufanyike kumchagua msimamizi.
  3. Msimamizi aende kufungua mirathi mahakamani akiwa na:
    - Nakala ya uamuzi wa Mkutano wa ukoo.
    - Cheti cha kifo.
  4. Tangazo hutolewa na mahakama kwa muda wa siku 90. Kama haku na pingamizi, msimamizi huka-bidhiwa barua ya kumwakilisha na kulipa madeni na kugawa mali.
  5. Msimamizi kugawa na kurejesha nakala ya mgawo mahakamani ili jalada lifungwe.
- Barua ya usimamizi lazima itaje:
- Familia ya marehemu na anuani zao na ndugu waliokuwa wakimtegemea.
  - Idadi na Aina ya Mali iliyoachwa na marehemu.

## 6. MUHIMU

Msimamizi wa mirathi ni mdhamini tu wa kuchunga mali iliyoachwa na marehemu kwa madhumuni ya kuwagawia warithi halali wa marehemu.